



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TAARIFA KWA UMMA**

**MAJARIBIO YA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA**

**WAPIGA KURA KATIKA KATA YA KIBUTA WILAYANI**

**KISARAWE NA KIHONDA KATIKA MANISPAA YA**

**MOROGORO**

Ndugu Wananchi,

Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mamlaka iliyopewa chini ya Ibara ya 74 (6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, pamoja na majukumu mengine, ina jukumu la Kusimamia na Kuratibu Uandikishaji wa Wapiga Kura katika Uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano pamoja na Madiwani kwa upande wa Tanzania Bara.

Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 15(5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Kifungu cha 21(5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume inapaswa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mara mbili kati ya kipindi kinachoanza mara baada ya Uchaguzi Mkuu na tarehe ya uteuzi wa Uchaguzi Mkuu unaofuata.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya zoezi la uandikishaji wa Wapiga Kura kwa majaribio katika Kata ya Kibuta iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani na Kata ya Kihonda iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Mkoani Morogoro kuanzia tarehe 29 Machi, 2019 hadi taraha 04

Aprili, 2019. Lengo kuu la uandikishaji huu wa majaribio ni kuvijaribu vifaa na mfumo utakaotumika kuandikisha Wapiga Kura, pamoja na kubaini changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza wakati wa zoezi rasmi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura utakaofanyika hapo baadae.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 10(1) na (2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, na Kifungu cha 15(1) na (2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, mwananchi mwenye sifa zifuatazo ataandikishwa katika zoezi la uandikishaji wa majaribio:-

- Awe na umri wa miaka 18 au atatimiza umri wa miaka 18 siku ya Uchaguzi Mkuu unaofuata; na
- Awe raia wa Tanzania

Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 11(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, na Kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, mtu yeyote hatakuwa na sifa ya kuandikishwa kuwa Mpiga Kura:

- Kama yupo chini ya kiapo cha utii katika nchi nyingine mbali ya Tanzania:
- Iwapo chini ya Sheria yoyote ile inayotumika Tanzania amebainika kuwa hana akili timamu au yuko kizuizini kama mhalifu mwenye ugonjwa wa akili au yuko kizuizini kwa ridhaa ya Rais;
- Iwapo amehukumiwa adhabu ya kifo na mahakama yoyote ya Tanzania au anatumikia kifungo kinachozidi miezi sita, na
- Iwapo mtu amepoteza sifa za kuandikishwa kuwa Mpiga Kura chini ya masharti ya Sheria tajwa za Uchaguzi au Sheria nyingine yoyote inayotumika na inayohusu makosa ya uchaguzi.

Uandikishaji huu wa majaribio utafanyika katika vituo 20 vya kuandikisha Wapiga Kura ikiwa ni vituo 10 katika kila Kata tajwa.

Tume pia inawajulisha wakazi wa Kata hizo ambao walijiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mwaka 2015 kuwa wanaweza kutumia fursa hii kuhakiki taarifa zao katika Vituo walivyojiandikisha.

Katika uandikishaji huu wa majaribio, Vyama vya siasa vinaruhusiwa kuweka Wakala mmoja katika kila Kituo cha kuandikisha Wapiga Kura kwa lengo la kushuhudia na kujiridhisha juu ya taratibu zitakazotumika wakati wa Uboreshaji rasmi wa Daftari. Vilevile, kubaini changamoto zinazoweza kujitokeza wakati wa zoezi hili la majaribio ili ziweze kupatiwa ufumbuzi kabla ya zoezi rasmi la Uandikishaji.

Vyama vya Siasa vitawajibika kuwasilisha orodha ya majina ya Mawakala na Vituo walivyopangiwa kwa Maafisa Waandikishaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. Aidha, Vyama vya Siasa vinatakiwa kuanzia sasa kuwasilisha nakala mbili za barua za utambulisho za kila Wakala kwa Maafisa hao zikiwa na picha mbili na nakala mbili za Kitambaulisho cha Taifa au Kadi ya Mpiga Kura, au Pasi ya kusafiria au Leseni ya Udereva.

Ikumbukwe kuwa kila chama kitagharamia wakala wake.

Wakati wa zoezi hili la Uandikishaji wa majaribio, Tume itatoa Elimu ya Mpiga Kura ili kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi. Njia

zitakazotumika ni pamoja na Runinga, Redio, Mitandao ya kijamii na magari ya matangazo.

Kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi niwaombe wakazi wa Kata za Kibuta iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe na Kata ya Kihonda iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kujitokeza kwa wingi katika Uandikishaji huu wa majaribio na pia kutoa ushirikiano kwa Tume wakati wote wa utekelezaji wa jukumu hili muhimu kwa mustakabali wa Demokrasia ya Taifa hili.

Imetolewa leo tarehe 25 Machi, 2019.

Jaji (R) Semistocles S. Kaijage

**MWENYEKITI**

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**